# Kufanya Kazi na Nchi

***Leo, nchi zenyewe, na sio Benki, zinaendesha ajenda za mipango yao, na usaidizi wa kiufundi kutoka kwa wafanyikazi wa Benki ya Dunia.***

Mikopo na Karadha  Uwezo na Usimamizi

Mbinu za muhimu zinazo ongoza uamuzi wa Benki katika nchi ni umasikini na utekelezaji, ikilenga kupeana kwake kwa mikopo katika nchi ambazo zina hali ya sera inavutia mafanikio ya usaidizi na pia ambako kuweko kwa Benki kutakuwa na manufaa makubwa.

Kuyafikia Malengo ya Millennium ya Maendeleo—ama kutumia msaada aina yowote kwa ukamilifu—kunategemea uwezo na ukamilifu wa mbinu za maendeleo za kila nchi pamoja na kiasi cha kujitilea kwake kwa maendeleo. Umilikaji wa nchi ni uti wa Mpango wa Pamoja wa Maendeleo (CDF) ya Benki na huongoza uhusiano kati ya Benki na mteja. Kila mbinu lazima ibuniwe kwa sera, taasis, na usimamizi mzuri, yote yanayosaidiwa na ongezeko la usaidizi wa maendeleo na ushirikiano wa kimataifa ulio imarika.

Country assistance strategies (CAS) [Mbinu za Usaidizi wa Nchi] zinaeleza kwa urefu uhusiano kati ya Benki na kila nchi inayo pokea mkopo. CAS, ambayo kwa kawaida huchukua mda wa miaka mitatu, hutambua kiwango na hali ya usaidizi utakao peanwa kulingana na mahitaji.

**Mipango ya Kukopesha**
Katika *Inchi zenye pato la chini*, ambazo zinastahili kupata karadha na mikopo isiyokuwa na riba kutok kwa International Development Association (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo], haki za CDF lazima zifwatilie katika mpango wa Poverty Reduction Strategy Paper (PRSP) [Mkakati wa Mbinu za Upunguzaji Umasikini] kabla kuandaliwa mpango wowote wa usaidizi wa Benki. Tangu mwaka 1999, PRSP—ambazo lazima zifanye upunguzaji wa umasikini kuwa kiini cha mipango yoyote ya maendeleo na ni lazima zijumuishe kikamilifu washirika kama vile sekta ya kibinafsi na utumishi wa umma—zimehitajika kwa ufadhili na misaada ya aina nyengine, kama inavyo stahili, upunguzaji wa madeni pia.
Kwa kuwa upunguzaji wa madeni ni jambo muhimu katika nyingi za nchi zenye pato la katikati (770k pdf), Benki, kupitia kwa mikopo ya IBRD, ina jukumu kubwa. Kwa kawaida huwa ni kufanya kazi ya kuhakisha kuweko kwa hali ya uwekezaji itakayoweza kuvutia msaada wa kibinafsi na kusaidia kuweko kwa mipango ya matumizi bora ya kijamii na yenye kuhakisha kuweko kwa rasilimali ya kibinadamu na kuimarisha usawa wa kuwa na uwezo wa kiuchumi.

***Kiasi cha kutosha cha masikini ulimwenguni wanaishi katika nchi zenye pato la kati, na ni ambao wana uwezo wa kufikia kwa masoko ya kimataifa ya fedha, ingawa kawaida ni chache na siyo yenye kudumu.***

**Msaada Usiokuwa wa Mikopo**
***Wanaoomba mkopo hupata mikopna na usaidizi usiokuwa wa mikopo kwa miradi ambayo imetambulika kuwa ya manufaa katika juhudi zao za maendeleo.*** Shughuli za kiuchumi na za sekta zimepangwa ili kupatikane kuelewa kikamilifu shida za maendeleo za wanaomba mikopo, za mahitaji na kuweko kwa uadhamini wa kando, na ukaguzi wa mbinu za maendeleo na shughuli za usaidizi wa wafadhili. Lengo muhimu la kazi ya kiuchumi na sekta ni kutambua kwa mapema miradi yenye manufaa makubwa ambayo masikini watakao faidika nayo kikamilifu.

***Kazi ya Benki ya kiuchumi na sekta inapeana msingi wa ukaguzi kwa ushauri za Benki ama sera na matumizi ya umma—na kwa maendeleo ya miradi na shughuli nyengine.***

***Karadha ni sehemu muhimu ya shughuli za Benki za maendeleo.*** Mbali na karadha zinazopeanwa kwa kupitia kwa IDA, Benki huwa na mipango ya karadha karibu kumi na miwili pamoja na hazina za amana 850 zinaopeana bilioni $1 kwa mwaka.
***Usaidizi wa dharura unapatikana baada ya mkasa ama tokio lolote lenye madhara kwenye uchumi na ikiwa unahitaji kushughulikiwa kwa haraka.*** Usaidizi huu unaweza kuwa wa namna aina mbalimbali. Kwa mfano, Benki inaweza kubuni mpango wa urekebishaji na inaweza kugeuza stakabadhi za mkopo uliopeanwa ili kusaidia marekebisho. Benki pia hupeana mikopo ya marekebisho ya dharura yenye

maregesho ya haraka. Kwa mfano, hivi karibuni Benki ilipeana milioni $160 kwa Ethiopia, Malawi, na Zambia kwa kukabiliana na ukame. Benki Ilipeana milioni $600 kwa India kwa marekebisho baada ya mtetemko wa ardhi Gujarat Januari 2001.
Benki pia hupanga miradi ya usimamizi kwa majanga—kwa mafano, utekelezaji wa mbinu za kuzuia mafuriko na moto wa misitu. Tangu mwaka wa 1980, Benki ya Dunia imeidhinisha zaidi ya operesheni 500 zinao husu majanga, yenye thamani ya zaidi ya bilioni $38.
***Kuzuia vita na marekebisho ya baada ya vita* ni muhimu kwa kupunguza umasikini.** Jukumu la Benki katika suhghuli hii limekuwa kubwa zaidi kushinda lile la urekebishaji wa baada ya vita. Sasa linajumuisha kazi ya kufufua uchumi, kupeana uwezo, maendeleo ya jamii, kuondoa mabomu ya ardhini, kuondoa majeshi na kuwasaidia wapiganaji kuregea katika maisha ya jamii, na kuwashughulikia wakimbizi.

***Wakati wa mwaka 1990 hadi 2002 peke yake, kulikuwa na vita 56 vya utumiaji silaha katika sehemu 44 tofauti ulimwenguni, vilivyozidisha umasikini na kusumbua juhudi za maendeleo.***

Juhudi za hivi karibuni za kushughulika na hali ya vita ni:

- Kusaidia urudishaji sawa wa usimamizi wa umma, elimu, na marekebisho ya miundombinu Afghanistan (milioni $368);
- Multisector Rehabilitation and Reconstruction Program [Mpango wa Kurudisha sawa na Marekebisho ya Sekta Mabalimbali] wa milioni $454 katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuisaidia hiyo nchi kuimarisha mazao ya kilimo na kupatikana kwa chakula, kurudishwa sawa kwa miundombinu muhimu na huduma muhimu za jamii, na kudumisha uwezo wa serikali kubuni na kutekeleza mipango yake ya maendeleo.
- Kusaidia kuondoa majeshi na kuwasaidia wapiganaji kuregea katika maisha ya jamii katika nchi kama Cambodia, Chad, Djibouti, Ethiopia, Mozambique, Sierra Leone, na katika Great Lakes Region [Sehemu Ya Maziwa Makubwa]; na pia kuregeshwa kwa watu waliohamishwa huko Azerbaijan, Liberia, Rwanda, na Sierra Leone.
- Kusaidia mipango ya mabomu ya ardhini huko Azerbaijan, Bosnia, Croatia na Ethiopia, ikilingana na maelekezo ya Benki ya kudhamini utoaji wa mabomu ya ardhini.

Pamoja na karadha za IDA, karadha za wafadhili mbalimbali zilio idhinishwa na Benki, na namna nyengine spesheli za usaidizi, Post-Conflict Fund (PCF) [Hazina ya Baada ya Vita] ya Benki huandaa kuweko kwa pesa za karadha—milioni $53 za karadha latika nchi 48 tangu mwaka 1997, zikiwemo:

- Afghanistan, mpango wa marekebisho pamoja na wafghani na ushirikiano wa wahusika wengine, mradi wa kuwapa uwezo jamii na mpango wa kusaidia sekta.
- Kurudisha sawa kwa sekta ya afya katika Somalia, kuliko tekelezwa na International Federation of the Red Cross [Shirilka la Kimataifa la Msalaba Mwekundu].
- Usaidizi mpya wa mpango wa afya ya bongo wa Travnik Bosnia ukishughulikia matatizo ya kibongo na kijamii ya vita.
- Kurudisha sawa mpango wa mawasiliano ya mashambani katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

***Kusisitiza kuweko kwa maendeleo yenye kuendeshwa na nchi kumesabibisha kusistizwa kwa kupeana uwezo katika nchi.*** Kubadili mawazo kuhusu maendeleo- ili yawe kamili, ya kuendeshwa na nchi zenyewe, hali ya kuwajibika na yakuweza kukaguliwa—kunahitaji uwezo ambao haukuweko awali. Rasilimali nyingi zaidi za Benki zinatumiwa kuimarisha uwezo wa nchi kusimamia maendeleo yao wenyewe. Hii ni aina moja ya “knowledge sharing” [kugawiana ujuzi] na umesababisha kuwa na namna mpya za kufanya kazi—haswa kwa shughuli za ushirika amabazo maofisa waseriakli, mawakilishi wa NGO na wa sekta ya kibinafsi, na wale wa serikali ya ufadhili wanakuwa pamoja katika mshilkano unaogawania ujuzi na taarifa, na kwa hivyo unaweza kubuni miradi ambyo kwa kweli inamilikwa na serikali yenye kujitolea.
Benki inazidi kusaidia juhudi hizo kwa mipango mipya inayo husisha ufundi. Kwa mfano, Global Development Learning Network [Mtandao wa Elimu ya Maendeleo], imeiwezesha kufikikia washiriki 45,000 wa serikali na sekta ya kibinafsi katika 2001. Development Gateway [Mlango wa Maendeleo] pia huandaa namana ya kupata taarifa—zenye maelezo kuhusu shughuli 300,000 ulimwenguni zilizo pata msaada wa wafadhili. World Bank Institute [Taasisi ya Benki ya Dunia] imeanzisha programu kadhaa zilizopangwa kwa mada, zenye nia ya kuimarisha uwezo.
Benki ilisaidia Global Development Network [Mtandao wa Maendeleo ya Ulimwengu], inayojumuisha taasisi za utafiti katika nchi zilizoendelea na zile zinazondelea na hukakisha kwamba matundu yanazibwa katika

kufanya utafiti ju ya ajenda ya kupunguza umasikini. African Virtual University [Chuo Kikuu cha Afrika cha Kwenye Mtandao] kinafanya kazi na vyuo vikuu vya Afrika, kwa kuzisaidia kuboresha hadhi zao na kuongeza idadi ya rasilimali ya kibinadamu yenye ujuzi katika bara hilo. Katika nyanja ya ufundi infoDev husaidia miradi midogo ya majaribio iliyopangwa kupunguza tofauti ya ujuzi wa matumizi ya vyombo vya kompyuta. World Links for Development [Mitandao ya Dunia wa Maendeleo] huwaleta pamoja walimu na wanafunzi wa shule za upilli katika nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea, na huwasaidia walimu na wanafunzi wajumuishe ufundi katika elimu.

**Kupunguza Ufisadi**

***Utawala.*** Ili udhamini wa nje utumike vyema ili kupunguza umasikini, ni lazima utumiwe kwa uwaminifu kamili. Tangu 1996 Benki imeanzisha zaidi ya mipango dhidi ya ufisadi 600 na juhudi za kiserikali katika zaidi ya nchi wateja100. Mwelekeo wa Benki unaelzwa katika mkakati wake wa mpango wa utawala na sekta ya umma, Reforming Public Institutions and Strengthening Governance: A World Bank Strategy [Mageuzi ya Taasisi za Kijamii na Kuimarisha Utawala: Mpango wa Benki ya Dunia]

***Karibu robo ya miradi yote sasa inajumuisha viungo vya matumizi ya umma na mageuzi ya kifedha.***

Wakati mwaka wa 1980, asilimia 0.6 pekee ya mikopo ya Benki ilikwenda kwa kusaidia mageuzi ya ndani ya sekta ya umma, kufikia mwaka wa fedha wa 2000 kiasi hichi kiliongezeka na kufikia asilimia 16. Kiasi cha miradi mipya yenye viungo vya matumizi ya umma kilipanda kutoka asilimia 9 kwa mwaka wa fedha wa 1997 hadi asilimia 23 kwa mwka wa fedha wa 2000. Wakati huohuo, kiwango cha mikopo ya marekebisho yenye viungo dhidi ya ufisadi ama uaminifu na fedha kinakidiriwa kuwa kilizidi kutoka asilimia 8 kwa mwaka wa fedha wa 1998 hadi asilimia 50 kwa mwaka wa fedha wa 2000. Baadhi ya mifano ya hivi karibuni ya miradi dhidi ya ufisadi ni:

- Usaidizi wa mageuzi ya ushuru Columbia na Venezuela
- Mageuzi ya kisheria Slovakia
- Mageuzi ya Mishiko ya Biashara Urusi na Ukraine
- Mageuzi ya usimamizi na utumishi wa umma Tanzania na Yemen
- Mageuzi ya jumla ya usimamizi Latvia na Cambodia
- Mageuzi ya matumizi ya umma na usimamizi wa fedha Burkina Faso, Ghana na Malawi.

Mbali na hayo, Benki imefanya ukaguzi maalum wa nchi zenyewe—kukiwemo utafiti wa kufwatilia matumizi ya fedha, na za watumishi wa umma—Albania, Argentina, Cambodia, Georgia, Latvia, Romania, Slovakia, Ecuador na Uganda.

***Kuzuia ufisadi katika miradi Inayodhaminiwa na Benki ya Dunia.***

Kulingana na mpango wa kukabilina na ufisadi wa 1997, Benki ilichukua mwelekeo wa kisiasa kabisa kuhusiana na uratibu wa ndani, ambayo kwa sasa inatumiwa na mashirika ya kifedha. Sasa Benki inakagua athari kuu pamoja na uratibu wa ndani.

Kurahisisha uwezo wa wafanyikazi kuripoti ufisadi, Benki imeweka mpango wa simu ya kimataifa isyokuwa na malipo ya huduma ya masaa 24 kwa kila siku yakuripoti kwa siri ufisadi: 1-800-831-0463.

Hadi Septemba 2001 uchunguzi wa Benki ulisababisha mashirika na watu 72 kupigwa marufuku kupata kandarasi zinazo dhaminiwa na Benki. Benki ya Dunia ndiyo Benki ya kwanza ya maendeleo ya shughuli mbalimbali kuchapisha katika mtandao wake, majina ya mashirika na watu waliopatikana kuwa na visa vya ufisadi ama udanganyifu fulani.